

Learning by Ear 2010 “Against the Current” – Urban Exodus

Episode 10: “Very good news”

Author: Alfred Dogbé

Editor: Yann Durand

Translator: Anne Thomas

WAHUSIKA:

Onyesho la 1:

- **JOURNALIST**
- **KABO** (UMRI WA MIAKA 57)
- **BAKI** (UMRI WA MIAKA 26)
- **ZEINA** (UMRI WA MIAKA 24)
- **NANA** (UMRI WA MIAKA 22)
- **TINGO** (UMRI WA MIAKA 32)

Onyesho la 2:

- **BEN** (UMRI WA MIAKA 29)
- **HADIA** (UMRI WA MIAKA 45)
- **HADARI** (UMRI WA MIAKA 48)

Onyesho la 3:

- **BEN** (UMRIWA MIAKA 29)
- **BAKI** (UMRI WA MIAKA 26)
- **ZEINA** (UMRI WA MIAKA 24)
- **THE CROWD** (WATU KWENYE DISKO)

Intro:

Karibu kwenye *Learning by Ear* katika mfululizo wa vipindi vyetu uitwao "Kukabiliana na Wimbi la Mabadiliko" kuhusu uhamiaji mijini.

Katika vipindi vilivyopita tumefuatiliza masaibu ya Ben pamoja na marafiki zake wawili ambao hawana ajira lakini walio na shahada za chuo kikuu ambao wameamua kuanzisha chama cha ushirika cha ukulima kijijini mwao.

Kwenye kipindi hiki cha kumi na cha mwisho, tutagundua kwamba ingawa mradi wao umekabiliana na matatizo aina mbalimbali, unalekea kuleta manufaa. Hizi ni "Habari njema".

Scene One: At Ben's.**JOURNALIST, BAKI, ZEINA, NANA, KABO AND TINGO.****1. ATMO: CRICKETS, HENS, POUNDING IN THE DISTANCE**

2. JOURNALIST (voice from the radio) Hizo ndizo habari za hivi karibuni kutoka kwenye soko la hisa ambazo umeletewa moja kwa moja na Matip Kerare kutoka mjini. Sasa tunakuletea habari za biashara.

Kulingana na taarifa ya chama cha wafanyibiashara, mauzo ya zao la njugu nje ya nchi yatahuka kwa asilimia 80 siku chache zijazo. Watu wanachelea kwamba hili litakuwa pigo kubwa kwa wakulima na lita...

3. ZEINA Ebu sikizeni!

(The lines 5 and 6 are spoken while the text in italics is being read)

4. JOURNALIST ...aathiri maisha ya wakazi. Shirikisho la wakulima limesema litakoma kuwasilisha mazao yote hadi pale wakuu wa serikali watakapohakikisha kwamba serikali imegharamia hasara na gharama za uendeshaji wa shughuli hiyo ya kilimo. Hasa wakati wa kipindi cha mpito ambacho tume itaeleza...

5. ZEINA Wanazungumzia kiwango cha njugu ...

6. BAKI Zeina tafadhali izime hiyo redio. Tuna kazi ya kufanya!

7. SFX: SOUND OF ON/OFF BUTTON ON THE RADIO

8. KABO Simwoni Ben.

9. ZEINA Yuko wapi?

10. NANA Je, kuna mtu kamuona tangu asubuhi?

11. **BAKI** Tufanye nini?
12. **NANA** Lazima tumsubiri.
13. **KABO** Kikao cha kwanza cha mafunzo ni kesho.
14. **ZEINA** Kwani mkutano huu umeshafunguliwa rasmi?
15. **KABO** Mnakubali tuanze mkutano bila Ben kuwepo? Inanibidi niende kumuona Hadari. Atanza kazi yake mpya kesho.
16. **ZEINA** Naona bora tumngoje Ben.
17. **BAKI** Tunaweza kuendelea na mkutano. Tupo wanne hapa, mmoja tu ndiye hayupo – hii ni idadi tosha ya kuwa na kikao kulingana na taratibu zilizowekwa.
18. **ZEINA** Nilitaka kuzungumzia suala muhimu na Ben ndiye anayehusika moja kwa moja na jambo hilo.
19. **KABO** Kweli?
20. **BAKI** Jambo gani hilo?
21. **NANA** Mbona hutuelezi wazi!
22. **ZEINA** Nina sababu zangu... Sisemi lolote kama Ben hayupo.
23. **BAKI** (Annoyed sigh)
24. **SFX: STEPS APPROACHING**
25. **BAKI** Huyo yuaja!
26. **SFX: KNOCKING AT THE DOOR**

27. **TINGO** (behind the door) Wenyewe wamo?
28. **KABO** Nani huyo?
29. **SFX: A CHAIR BEING PUSHED BACK, STEPS GOING TO THE DOOR, A DOOR GRATING**
30. **TINGO** ... Alaa! Hujambo Baki!
31. **BAKI** Unamtaka nani? Tuna mkutano.
32. **TINGO** Ningependa kuwa mwanachama wa chama cha ushirika.
33. **EVERYONE** Ati nini????
34. **TINGO** Nimezisoma kanuni za chama. Ninaweza kuwa mshirika.
35. **BAKI** Umesoma na kufahamu kuwa chama kina haki kuwakatalia maombi ya uanachama watu fulani.
36. **TINGO** Nisikize, najua hamtilii maanani kazi yangu wala hamningatii mimi... Ninajua hivyo... lakini ningependa kuwapa pendekezo fulani.
37. **NANA** Tena?
38. **TINGO** Ndiyo. Lakini mara hii ni la dhati, linalovutia na lenye faida.
39. **ZEINA** Unampendekezea nani?
40. **TINGO** Ninawahitaji. Labda mmeshasikia kwamba thamani ya njugu imeshuka kabisa.
41. **BAKI** Hilo halituhusu sisi.

- 42. TINGO** Nimejitolea. Tayari nimepata arabuni ya msimu ujao. Nitapoteza kiasi kikubwa cha fedha. Kiasi kikubwa.
- 43. BAKI** Hujajibu swali langu. Haya yote yanatuhusu vipi?
- 44. TINGO** Ninakabiliwa na tatizo, na ninatafuta suluhisho. Na suluhisho bora zaidi naona niwahusishe ninyi.
- 45. BAKI** Na kwa nini tujihusishe?
- 46. TINGO** Ni faida kwa kila anayehusika. Kila mtu – chama, wakulima, kijiji kizima, na mimi...
- 47. NANA** Kimsingi unatuhitaji sisi ili usipate hasara kubwa.
- 48. TINGO** Ndiyo. Lililobaki kwangu mimi ni kuzitumia hizo huduma za chama cha ushirika. Chama chenyewe kinaweza kuwapatia wanachama wake wafanyikazi wenye uzoefu mkubwa.
- 49. BAKO** Unadhani si ni watumwa? Maanake tukufanyie wewe kazi ili uendelee kutupunja unavyotaka?
- 50. TINGO** Sivyo hivyo. Siwezi kukosa kukuza njugu. Si mwaka huu. Mimi huwalipa wakulima nusu ya deni lao wanapomaliza kazi kisha huwalipa nusu iliyobaki baada ya mavuno kuuzwa. Lakini mwaka huu hilo hawatalikubali.

- 51. NANA** Ndiyo! Kwa sababu kabla ya tatizo hili kuzuka, tuliwahamasisha kudai malipo yao kamili mara tu wanapokamilisha kazi zao.
- 52. TINGO** Napendekeza niwalipe theluthi ya malipo yao miezi miwili kabla ya msimu kuanza, theluthi nyingine wanapomaliza kazi, kisha ya mwisho baada ya kuyauza mazao. Chama kitasimamia haki zao. Mambo yakienda kombo mnaweza kunishtaki na si wao.
- 53. BAKI** Nasi tunahusika vipi?
- 54. ZEINA** Ebu tumsikilize, Baki! Nini tatizo kuu la wakulima?
- 55. TINGO** Hawana fedha za kutosha uhakika wa mavuno mazuri.
- 56. ZEINA** Lakini wakipata kiasi fulani cha fedha sasa na tushirikiane nao, wataongeza kilimo cha mazao ya chakula.
- 57. TINGO** Tunaweza kuanzisha ushirikiano – shamba langu, chama na wakulima. Tunaweza kutatua tatizo la upungufu wa chakula na kuondoa umaskini.
- 58. KABO** Vipi tunavyoweza kutekeleza hayo?
- 59. TINGO** Nawaahidi kubadili uzalishaji wangu haraka iwezekanavyo: sitaki tena kilimo cha aina moja ya zao la chakula. Nitakigawia chama sehemu fulani ya ardhi yangu... Pia nitauza vipande vya ardhi kwa bei nafuu! Kwa hali hiyo baadhi ya wakulima watahughulikia kilimo chao kwa uhuru wautakao. Tunahitaji tu kujadiliana jinsi ya kutekeleza.

60. **KABO** Karibu ukae!

----- MUSIC -----

Scene two: Village bar.

BEN, HADIA, HADARI

61. **ATMO: VILLAGE BAR. LOUD DANCE MUSIC; CONVERSATION IN THE BACKGROUND**

62. **BEN** **(SHOUTING)** Kwani hawezi kupunguza sauti ya muziki?

63. **HADIA** **(SHOUTING)** Wasemaje?

64. **BEN** **(SHOUTING)** ... Sauti ya muziki! ... **(VOLUME DECREASES)** ... mfyuu!

65. **HADIA** Inaonekana kwamba hali leo jioni itakuwa ni raha tele!

66. **HADARI** Natumai hivyo! Kijiji kizima kitakumbuka daima karamu hii!

67. **HADIA** Hatutakusahau, Hadari. Miaka minane ni muda mfupi!

68. **HADARI** Ninajua. Lakini hamtanikumbuka kwa mazuri tu. Hapa pia nina maadui...

69. **HADIA** Hilo ni kawaida kwa kila binadamu. Muhimu zaidi ni hao marafiki uliowapata.

70. **BEN** Na tuko wengi sana. Unajua hivyo bila shaka.

71. **HADARI** Usemayo ni kweli, na kwa hilo ninakushukuru, Ben.
72. **BEN** Hata, hakuna kubwa nililotenda...
73. **HADARI** Wajua nini, sasa hivi ningependa nistaafu mapema kama ulivyofanya ... Ndiyo... nirudi kijijini kwetu nami nikaanzishe chama cha ushirika wa kilimo.
74. **BEN** Wazo zuri hilo! Tunaweza kushirikiana!
75. **HADARI** Wajua, maisha yangu yamebadilika sana tangu uliporejea hapa. Najihisi nilibahatika sana kujuana nawe. Asante sana.
76. **BEN** Sidhani ... kusema kweli, ni...
77. **HADARI** Ukweli! Nimeamua nikujulishe hayo na nitayarudia wakati wa karamu ili watu wote wapate kuyasikia.
78. **HADIA** Yaache hayo! Utaniliza! Usizungumze kama mtu ambaye unaondoka milele! Hii ni sherehe si mazishi!
79. **HADARI** Umesema kweli, Hadia! Watu wanahitaji kupata muda wa kujiburudisha leo usiku!
80. **BEN** Usitie shaka. Baa hii ni yetu usiku kucha. Vinywaji tayari vimepata baridi. Na muziki nao unapigwa kwa sauti ya juu!
81. **HADIA** Sijacheza muziki kiasi miaka kumi na mitano iliyopita.
82. **HADARI** Tafadhali, subiri hata muda ufike ili nicheze nawe!
83. **HADIA** Sawa!
84. **BEN** Nitaona wivu!

85. **HADIA** Kwa nini? Kwani Nana hahudhuria hafla hii?
86. **BEN** Bado hana habari kuhusu hafla hii... lakini atakuja tu...
Nina hakika...
87. **HADARI** Hilo ndilo tatizo. Hakuna aliye na habari za hafla hii. Kweli watu watahudhuria?
88. **BEN** Tilitaka iwe jambo la kushtukiza. Usiwe na wasiwasi.
Tutawaalika watu wachache sasa.
89. **HADIA** Nitawaomba wanawake pamoja na wasichana wote kuwaleta wanaume wote.
90. **BEN** Haya, ninaondoka! Tayari nimechelewa kuhudhuria mkutano wa chama. Tutaonana baadaye!
91. **HADIA & HADARI** Tutaonana baadaye!
92. **SFX : STEPS GOING AWAY**

----- MUSIC -----

Scene three: Bar.

BEN, BAKI, ZEINA, THE CROWD

93. **SFX: IN A BAR. PARTY ATMOSPHERE, LOUD DANCE MUSIC, SHOUTS, LAUGHTER, BOTTLES AND GLASSES**
94. **BEN** Hadari si haba kwa kucheza muziki.
95. **ZEINA** Basi ni ajabu na umri huo wake!

96. **BEN** Anajihisi kijana bado!
97. **SFX: LOUD CLAPPING**
98. **THE CROWD** Hongera! Hongera!
99. **SFX: STEPS COMING**
100. **BAKI** Zeina! Ben! Nimewaitea vinywaji!...
101. **BEN** Hatimaye! Ulitaka kusema nini vile?
102. **BAKI** Subiri... Tutafute mahala pengine penye utulivu kiasi.
103. **SFX: STEPS, THE MUSIC GETS QUIETER**
104. **ZEINA** Wewe, Baki! Mwambie!
105. **BAKI** Tafadhalini!
106. **SFX: GLASSES ARE RAISED AND CLINKING SOUNDS**
107. **BEN** Kuna nini?
108. **BAKI** Ningependa kuwatangazia huyu hapa Zeina, mke wangu wa siku za usoni!
109. **BEN** Mta... mtafunga ndoa?
110. **ZEINA** Naam Ben! Baki anataka kubaki hapa kijijini ili asaidie kukiimarisha chama chetu cha ushirika.
111. **BAKI** Kijiji kinabadilika kwa kasi na nadhani maisha ya siku zijazo huenda yakawa mazuri! Hata Tingo ameunga mkono wito wa kutunza mazingira na hasa mazao ya chakula!

- 112. ZEINA** Ni jambo la kuridhisha, Ben! Hatimaye wanakijiji hawana haja ya kwenda mbali kununua viazi vikuu, mtama, mawele na mboga za bei ghali! Watazikuza wao wenyewe.
- 113. BAKI** Na zaidi ya hayo, watauza mavuno ya ziada watakayopata!
- 114. BEN** (**looking a bit absent-minded**) Hilo ni kweli... jambo la kufurahisha sana... tayari sisi tumekuwa mfano wa kuigwa katika eneo letu... Lakini...
- 115. ZEINA** Una nini Ben?
- 116. BAKI** Hujamakinika...
- 117. BEN** Eee... Hapana... hapana! Nipe dakika moja, naja sasa hivi...
- 118. SFX: RAPID STEPS GOING AWAY**
- 119. BEN** (**Going away**) Ninakwenda kumchukua Nana...mimi pia ninalo tangazo linalomhusu!

Outro:

Na huu ndio mwisho wa kipindi cha mwisho cha "Kukabiliana na Wimbi la Mabadiliko", mfululizo wetu wa Learning by Ear kuhusu uhamiaji mijini. Tunatumai kwamba wengine watashawishika kama vile Ben, Zeina na Baki wanaotaka kujaribu bahati zao kikazi nje ya miji.

Mtunzi: Alfred Dogbé

Pamoja na sauti za:

Na mafundi wa mitambo:

Na usaidizi wa:

Na wahariri:

Na watayarishaji:

Ikiwa unataka kukisikiliza tena kipindi hiki au kutuletea maoni kuhusu mada zilizoshughulikiwa, tafadhali fungua ukurasa wa tovuti www.dw-world.de/lbe au tulettee barua pepe kupitia anwani yetu lbe@dw-world.de.

Asante sana kwa kutusikiliza. Kwaheri!

END OF EPISODE 10